Yesu Akaendelea Mbele Kidogo

na

Ellis Forsman

Yesu Akaendelea Mbele Kidogo

na

Ellis Forsman

Oktoba 12, 2011

Yesu Akaendelea Mbele Kidogo

Mat. 26:39

Mat. 26:39, "*Akaendelea mbele kidogo, akaanguka kifudifudi, akaomba akisema Baba yangu, ikiwezekana kikombe hiki kiniepuke; walakini si kama nitakavyo mimi, bali kama utakavyo wewe.*"

Sehemu ya kwanza ya kifungu hiki kinaunda kichwa cha somo letu.

Kinachothibitishwa hapa kwa Yesu kinaweza pia kuthibitishwa katika kila uhusiano wa maisha, na katika uwepo wa mwanadamu.

Dhana hii kwa mara moja inamtofautisha Yesu na kiongozi mkuu yeyote ambaye amekua mbele yetu. Musa, Ibrahimu, Yohana mbatizaji, na Paulo waliendelea mbele kidogo kuliko wengi wetu wanavyoweza kwenda. Yesu aliendelea mbele sana. Anafahamu makosa na udhaifu wetu, lakini alipenda aendelee mbele kidogo.

Vitu vilivyo sababisha Kristo aende mbele

Alienda mbele kwa upendo.

Anafundisha kwamba tunapaswa kupendana sisi kwa sisi. Yoh. 13:34, "*Amri mpya nawapa, mpendane. Kama vile nilivyowapenda ninyi, nanyi mpendane vivyo hivyo.*"

Hili ni rahisi, kwa sababu wote tunaweza kuwapenda wale tulionao na wale walio sababu ya kuwepo.

Anafundisha kwamba tunapaswa kuwapenda maadui zetu. Mat. 5:44, "*Lakini mimi nawaambia, wapendeni adui zenu, waombeeni wanaowaudhi,*"

Huu ni mtihani mgumu kwa mwanadamu. Mat. 5:39, "*Lakini mimi nawaambia msishindane na mtu mwovu; lakini mtu akupigaye shavu la kuume, mgeuzie na la pili.*"

Yesu alisema upendo uliomkuu ni mtu kuutoa uhai wake kwa ajili ya marafiki zake.

Yoh. 15:13, "*Hakuna aliye na upendo mwingi kuliko huu, wa mtu kuutoa uhai wake kwa ajili ya rafiki zake.*"

Katika hali fulani, watu wengi wangependa kufanya hili. Unaweza vyema kuutoa uhai wako kwa ajili ya mtoto wako, mwenzi wako, au rafiki yako wa karibu.

Yesu aliwafia maadui zake. Rumi. 5:6-10, "*Kwa maana hapo tulipokuwa hatuna nguvu, wakati ulipotimia Kristo alikufa kwa ajili ya waovu. Kwa kuwa ni shida mtu kufa kwa ajili ya mwenye haki; lakini yawezekana mtu kuthubutu kufa kwa ajili ya mtu aliye mwema. Bali Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi. Basi zaidi sana tukiisha kuhesabiwa haki katika damu yake tutaokolewa na ghadhabu kwa yeye. Kwa maana ikiwa tulipokuwa adui tulipatanishwa na Mungu kwa mauti ya Mwana wake; zaidi sana baada ya kupatanishwa tutaokolewa katika uzima wake.*"

Mwanadamu, kama mtawala, hawapendi kufanya hilo.

Yesu aliendelea kwa upendo.

Aliendelea kwa utii.

Alikuwa mtiifu kwa Mungu. Fil. 2:8, "*Tena alipoonekana ana umbo kama mwanadamu, alijinyenyekeza akawa mtii hata mauti, naam, mauti ya msalaba.*"

Utii wake ulienda hadi hatua ya kuutoa uhai wake.

Alikuja kufanya mapenzi ya Baba yake.

- Yoh. 4:34, "*Yesu akawaambia chakula changu ndicho hiki, niyatende mapenzi yake aliyenipeleka, nikaimalize kazi yake.*"
- Yoh. 6:38, "*Kwa kuwa mimi sikushuka kutoka mbinguni ili niyafanye mapenzi yangu, bali mapenzi yake aliyenipeleka.*"

Watu wengi hawawezi kumtii Kristo katika mafundisho yake. Mat. 6:33, "*Bali utafuteni kwanza ufalme wake, na haki yake; na hayo yote mtazidishiwa.*"

Yesu aliendelea mbele katika utii na akawa mwanzilishi wa wokovu wetu. Ebr. 5:8-9, "*Na ingawa ni Mwana, alijifunza kutii kwa mates ohayo yaliyompata; naye alipokwisha kukamilishwa, akawa sababu ya wokovu wa milele kwa watu wote wanaomtii.*"

Yesu aliendelea mbele kwa maombi.

Usiku wote aliutumia kwa maombi. Luka 6:12, "*Ikawa siku zile aliondoka akaenda mlimani ili kuomba, akakesha usiku kucha katika kumwomba Mungu.*"

Aliomba katika majaribu yo yote; aliomba katika kubadilishwa kwake.

Luka 9:29, "*Ikawa katika kusali kwake sura ya uso wake ikageuka, mavazi yake yakawa meupe yakimeta meta.*"

Aliomba alipokuwa anabatizwa. Luka 3:21, "*Ikawa watu wote walipokwisha kubatizwa na Yesu naye amebatizwa naye anaomba mbingu zilifunuka;*"

Aliomba baada ya kumponya mwenye ukoma. Luka 5:16, "*Lakini yeye alikuwa akijiepua akaenda mahali pasipokuwa na watu, akaomba.*"

Aliomba kabla hajawachagua wale kumi na wawili. Luka 6:12, "*Ikawa siku zile aliondoka kwenda mlimani ili kuomba, akakesha usiku kucha katika kumwomba Mungu.*"

Je unaongea na Mungu kabla hujafanya maamuzi makuu?

Aliomba msalabani kwa ajili ya wauaji wake. Luka 23:34, "*Yesu akasema Baba uwasamehe kwa kuwa hawajui watendalo. Wakagawa mavazi yake wakipiga kura.*"

Je unawaombea maadui zako?

Aliomba alipokuwa anakaribia kukata roho. Luka 23:46, "*Yesu akalia kwa sauti kuu akasema Ee Baba, mikononi mwako naiweka roho yangu.*"

Tunapaswa kuomba bila kukoma.

- 1 Thes. 5:17, "*Ombeni bila kukoma.*"
- Luka 18:1, "*Akawaambia mfano, ya kwamba imewapasa kumwomba Mungu siku zote, wala wasikate tamaa.*"

Tunaona kwamba Yesu aliendelea kwa maombi.

Yesu aliendelea mbele katika msamaha.

Alifundisha msamaha. Mat. 6:14-15, "*Kwa maana mkiwasamehe watu makosa yao, na Baba yenu wa mbinguni atawasamehe ninyi. Bali msipowasamehe watu makosa yao, wala Baba yenu hatawasamehe ninyi makosa yenu.*"

Yesu alitenda kile alichokifundisha. Luka 23:34, "*Yesu akasema Baba uwasamehe kwa kuwa hawajui watendalo. Wakagawa mavazi yake wakipiga kura.*"

Wachache hawawezi kwenda umbali huo.

Stefano na Paulo walifuata mfano wake.

- Mdo. 7:60, "*Akapiga magoti akalia kwa sauti kuu, Bwana usiwahesabie dhambi hii. Akiisha kusema haya akalala. Na Sauli alikuwa akiona vyema kwa kuuawa kwake.*"
- 2 Tim. 4:14-16, "*Iskanda mfua shaba alionyesha ubaya mwingi kwangu; Bwana atamlipa sawa sawa na matendo yake. Nawe ujihadhari na huyo kwa sababu aliyapinga sana maneno yetu. Katika jawabu langu la kwanza hakuna mtu aliyesimama upande wangu, bali wote waliniacha naomba wasihesabiwe hatia kwa jambo hilo.*"

Tunapaswa kujifunza tabia hii ya msamaha. Wengi wanataka kusamehe pasipo kusahau. Wengine hawawezi kusamehe kabisa.

Yesu aliendelea mbele kwa huzuni.

Isaya 53:3, "*Alidharauliwa na kukataliwa na watu; mtu wa huzuni nyingi ajuaye sikitiko; na kama mtu ambaye watu humficha nyuso zao, alidharauliwa wala hatukumhesabu kuwa kitu.*"

Yuko tayari kufahamu na kuhisi huzuni yetu, kwa sababu amepitia mengi.

Alilia pamoja na Mariam na Martha juu ya kifo cha ndugu yao Lazaro. Yoh. 11:35, "*Yesu akalia.*"

Alikuwa na huzuni hata mauti. Mat. 26:38, "*Ndipo akawaambia roho yangu ina huzuni nyingi kiasi cha kufa; kaeni hapa mkeshe pamoja nami.*"

Yesu aliendelea mbele kwa wema. Mdo. 10:38, "*Habari za Yesu wa Nazareti jinsi Mungu alivyomtia mafuta kwa Roho Mtakatifu na nguvu naye akazunguka huko na huko, akitenda kazi njema na wote walioonewa na ibilisi kwa maana Mungu alikuwa pamoja naye.*"

Maadui zake wasinge pata kosa ndani yake. Ni mtu pekee ambaye hakua na dhambi ambaye hajawahi kuishi. 1 Pet. 2:22, "*Yeye hakutenda dhambi, wala hila haikuonekana kinywani mwake.*"

Unaweza kuendelea naye kwa kiwango gani?

Watu elfu tano walimkaribia ili kula mikate na samaki. Mat. 14:21, "*Nao waliokula walikuwa wanaume wapata elfu tano, bila wanawake na watoto.*"

Je umewahi kuwa karibu na mkuu ili kula mkate wa uzima?

Sabini walimkaribia ili watumwe katika agizo lenye ukomo. Luka 10:1, "*Basi baada ya hayo Bwana aliweka na wengine, sabini*

akawatuma wawili wawili wamtangulie kwenda katika kila mji na kila mahali alipokusudia kwenda mwenyewe."

Je umewahi kumkaribia Bwana vya kutosha ili utumwe katika agizo kuokoa roho?

Kumi na wawili walikaribia vya kutosha ili kuwa mitume. Mitume walikuwa mawakili wa neno la Mungu.

Je wewe ni mpelekaji wa neno la Mungu?

Siku ya Pentekoste, 120 walikuwa karibu vya kutosha katika kuabudu na kusali. Mdo. 1:14, "*Hawa wote walikuwa wakidumu kwa moyo mmoja katika kusali pamoja nao wanawake, na mariamu mama yake Yesu, na ndugu zake.*"

Je uko karibu na yeye vya kutosha ili uabudu na kuomba?

Paulo alikuwa karibu na Yesu vya kutosha kuweza kumpa uhai wake kwake. 1 Kor. 11:1, "*Mnifuate mimi kama mimi ninavyomfuata Kristo.*"

Tunapaswa kumpa Yesu maisha yetu, pia. Fil. 1:21, "*Kwa maana kwangu mimi kuishi ni Kristo na kufa ni faida.*"

Je Kristo anamaanisha kiasi hiki kwako?

Yesu hakuacha

Yesu hakuacha...

- Kwa sababu Yuda alikuwa msaliti.
- Au kwa sababu Petro alikuwa na mashaka kwa wakati fulani.
- Hakuacha kuhubiri na kuishi sahihi kwa sababu baadhi ya ndugu zake hawakusamehe na hawakuwa wema.
- Hakuacha tu.

Wengine waliacha; je wewe? Kama uliacha, sababu ilikuwa nini?

Sababu ye yote unayoweza kutamka, Yesu angeweza pia kusema kama iyo hiyo. Alikuwa na kila sababu ya kukatishwa tamaa. Wanafunzi wake mwenyewe walikuwa wataratibu katika kujifunza. Maadui zake waliegama katika maangamizi yake.

Lakini hakuacha.

Kama mtoto, alisema katika Luka 2:49, "*Akawaambia kwani kunifuata? Hamkujua ya kuwa imenipasa kuwamo katika nyumba ya Baba yangu?*"

Wakati uhai wake hapa duniani ulipokuwa unakaribia kwisha, alimwambia Baba yake, Yohana 17:4, "*Mimi nimekutukuza duniani, hali nimeimaliza kazi ile ulionipa niifanye.*"

Hakuacha; alimaliza kazi yake.

Unapokaribia mwisho wa uhai wako, je waweza kusema, "Nimemaliza kazi ambayo Mungu alinipa niifanye"? Au utasukumwa kusema, "Nilianza, lakini nikaacha"? Je utasimama mbele ya kiti cha hukumu cha Mungu na kukiri kwamba ulikuwa muachaji?

Uzima wa milele umeahidiwa kwa wale watakao vumilia hadi mwisho. Mat. 10:22, "*Nanyi mtakuwa mkichukiwa na watu wote kwa ajili ya jina langu; lakini mwenye kuvumilia mpaka mwisho ndiye atakayeokoka.*"

Hakutakuwa na udhuru katika Siku ya Hukumu isipokuwa kama ulikuwa na maisha matakatifu yenye kuvumilia katika dunia hii.